

## UUNDAJI WA ISTILAHIZA KISIASA TANZANIA

H.J.M. Mwansoko

### 1.0 Utangulizi

Mwaka 1992 Tanzania ilipitisha sheria ambapo iliacha mfumo wa siasa ya chama kimoja na kuingia katika mfumo wa siasa ya vyama vingi. Hata hivyo mfumo wa vyama vingi halikuwa jambo geni kabisa nchini Tanzania kwani chaguzi za mwaka 1958, 1959, 1960 na 1962 zilishirikisha vyama vingi (taz. Nsekela 1965:173 - 175). Pamoja na hayo, vyama hivi vya mwanzo, ukiachilia mbali chama cha TANU, havikuwa na nguvu. Uongozi wake ulikuwa dhai fu na vilikuwa na wanachama wachache. Hivyo havikuweza kudumu kwa muda mirefu. Serikali ilipoamua kufuata mfumo wa siasa ya chama kimoja kunako mwaka 1963 (Nsekela 1965:196) hapakuwepo na kipingamizi chenyé uzito.

Lakini kurejeshwa kwa mfumo wa siasa ya vyama vingi mwaka 1992 kulikuwa na msisimko na kishindo kikubwa. Na hali hii inatokana na mwamko mkubwa wa kisiasa walio nao wananchi baada ya kujitawala kwa zaidi ya miongo mitatu. Hivyo idadi ya vyama vipyä vya kisrasa vilivyoanzishwa ilikuwa kubwa. Licha ya Chama cha Mapinduzi CCM, chama kinachotawala, vyama vipyä vifuatavyo vimeshasajiliwa rasmi: National Convention for Constitutional Reform (NCCR - Mageuzi), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Civic United Front (CUF), United Democracy Party (UDP), Tanzania Labour Party (TLP), National Popular Party (PONA), Union for Multiparty Democracy (UMD) United Peoples Democratic Party (UPDP), National League for Democracy (NLD), Tanzania Democratic Alliance (TADEA), National Reconstruction Alliance (NRA), na Tanzania Peoples Party (TPP). Vyama vyote hivi vina uongozi mzuri na wanachama wa kutosha. Aidha vyote vilishiriki katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 1995<sup>1</sup>.

Kuanzishwa upya kwa mfumo huu wa siasa ya vyama vingi hapa nchini na pia kushiriki kwa vyama hivi katika Uchaguzi Mkuu na chaguzi ndogo kadhaa kumepelekeea katika jitihada za kubuni msamiati mpya wa Kiswahili unaokidhi mahitaji ya mfumo ulioibuka wa kisiasa.

Lengo la makala hii ni kujadili kuhusu msamiati wa Kiswahili unoambatana na mfumo huu mpya wa kisiasa. Tutajadili juu ya maeneo ya mawasiliano ambamo msamiati umeundwa, mbinu zilizotumiwa katika kuunda msamiati husika, vyanzo vya msamiati huo na uthabiti wa msamiati uliobuniwa.

Uchunguzi huu una saida mbili kubwa. Kwanza, ni kuuweka katika rekodi msamiati wa Kiswahili unaotumika katika kuendeshea mfumo wa siasa ya vyama vingi nchini Tanzania kwa ajili ya rejea ya kudumu. Na pili, kuusambaza msamiati huo kwa nchi jirani (na nyinginezo) zinazotumia Kiswahili na ambazo ama tayari zinafuata mfumo wa siasa ya vyama vingi (kama Kenya) ama zina uwezekano mkubwa wa kufanya hivyo siku za mbele (kama Uganda). Hatua ya usambazaji itaimarisha juhudzi za usanifishaji wa msamiati huu kwa ngazi ya kanda ya Afrika Mashariki na Kati kwa vile itazuia mfumko wa visawe kwa dhana ambazo tayari zimeshapatiwa maneno nchini Tanzania.

### 2.0 Misingi ya Kinadharia.

Wanazuoni wa masuala ya usitawishaji wa misamiati na istilahi wameshæleza kuwa shughuli yoyote anayoifanya binadamu na pia fani yoyote ya maarifa huwa na idadi maridhawa ya dhana na

maneno (=msamiati,istilahi) yanayoziwakilisha dhana hizo.Maendeleo katika shughuli na fani hizo daima hupelekeea katika kuibuka kwa dhana mpya ambazo ni lazima zitafutiwe maneno ya kuziwakilisha(taz.Felber 1984). Utafutaji wa maneno hayo huweza kupata mafanikio iwapo:

- (i)Kasi ya maendeleo hayo itakuwa ya wastani,yaani si kubwa mno.
- (ii)Wanajamii - lugha wanaouhitaji msamiati husika mpya ndio watakaoshiriki katika kubuni na kuunda msamiati huo, na
- (iii) Kuna matumizi ya kutosha ya msamiati uliobuniwa mionganoni mwa wanajamiji-lugha yanayowezesha msamiati huo kusanifika na kutumiwa kwa hali ya ulinganifu.(Taz. Ferguson 1968:33).

Makala hii itaonyesha jinsi maendeleo katika medani ya siasa nchini Tanzania yalivyosababisha ubunifu wa istilahi mwafaka za Kiswahili, ubunifu uliofanywa na wanasiasa wenyewe ili kukidhi mahitajio yao ya kimawasiliano.Aidha tutaonyesha jinsi matumizi mapana ya msamiati huu yalivyopelekea katika usanifishaji wa mapema wa msamiati huo.

### **3.0 Mbinu za utafiti**

Data zinazotumika katika makala hii zinatokana na utafiti uliofanywa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma na katika Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, wakati wa vikao vyake vya bajeti vya mwaka 1996.Wakati wa utafiti huo tuliwahojii Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi juu ya itikadi za vyama vyao na mfumo wa uongozi wa vyama hivyo.Katika mahojiano hayo tulirekodi msamiati mpya wa Kiswahili ulioelezea itikadi na sera za vyama hivyo.Aidha tulifuatilia majadiliano ya Bungeni na katika Baraza la Wawakilishi ambapo pia tulipata maneno kadhaa mapya hasa yanayohusu nyadhifa za viongozi ndani ya Bunge na Baraza la Wawakilishi.

Licha ya utafiti huu wa-uwandani (au masikanini), tulikusanya pia data kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari vya humu nchini (yaani Tanzania). Tangu vuguvugu la siasa za vyama vingi lianzu kushamiri humu nchini, hususani baada ya mwaka 1992, tumekuwa tukisoma magazeti mbalimbali ya Kiswahili (k.m Uhuru, Mzalendo, Msanyakazi, Majira, Nipashe, Mtanzania, Rai...n.k.) na kuzirekodi katika kijidaftari kidogo data zinazohusiana na mada ya utafiti wetu. Data za aina hii zilirekodiwa pia kutokana na kusikiliza redio na kuangalia televisheni. Kipindi cha uandikishaji wa vyama vipyta vya kisiasa (1992 -1993) na wakati wa chaguzi ndogo na Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 1995 ndivyo viliviyokuwa hasa na mfumko wa msamiati mpya husianifu na mfumo wa siasa ya vyama vingi.

Uchanganuzi wa data zilizokusanywa ndiwo unaotumika kama "mhimili" wa mjadala wa makala hii.Na tuanze mjadala madhukura kwa kuainisha maeneo ya mawasiliano ambamo msamiati mpya wa siasa mamboleo ya vyama vingi umeibuka.

### **4.0 Kuibuka kwa Msamiati Mpya Husianifu na Siasa ya Vyama Vingi**

Mfumo wa siasa ya vyama vingi wa nchini Tanzania umeiga kwa kiwango kikubwa mfumo wa siasa ya aina hiyo wa Uingereza na, kwa kiwango kidogo, uie wa Marekani.Kwa hali hii dhana nyingi zinazohusu uendeshaji wa siasa za vyama vingi zimetokana na lugha ya Kiingereza inayotumika huko Uingereza na Marekani. Kwa vile nchini Tanzania shughuli za kisiasa zimekuwa zikiendeshwa kwa lugha ya Kiswahili kwa muda mrefu (taz. Mwansoko na Tumbo -Masabo 1996), wanasiassa wa Tanzania walilazimika kutafuta visawe vya Kiswahili kwa msamiati wa Kiingereza unaowakilisha dhana mbalimbali za mfumo wa siasa ya vyama vingi. Mathalani dhana ya "Kiongozi wa Upinzani (Bungeni)" imekopwa toka Bunge la Uingereza kwa maana ya "Leader of the Opposition". Hata hivyo,hii haimaanishi kuwa dhana zote husianifu na mfumo wa siasa ya vyama vingi zimekopwa toka kwenye lugha ya Kiingereza.Zipo dhana na msamiati ambazo zimeibuka kufuatana na hali halisi ya mazingira ya Tanzania.Mifano ya msamiati wa aina

hii ni: maskani, wakereketwa,wafurukutwa, n.k.<sup>2</sup>, ambao unataja mashabiki wa vyama mbalimbali nya kisiasa.

Maeneo muhimu ya mawasiliano ambamo msamiati mpya wa kisiasa umeibuka ni pamoja na yale yanayohusu itikadi,falsafa na sera za vyama, uungwaji mkono wa vyama,kampeni wakati wa chaguzi,nyadhifa mbalimbali vyamani na katika vyombo nya uwakilishi.Tutavijadili vipengele hivi kwa kina hapa chini.

#### **4.1 Msamiati unaohusu itikadi, falsafa na sera za vyama.**

Uwanja wa itikadi na sera umezalisha maneno machache mapya, bila shaka kutokana na kutokuwepo kwa tofauti kubwa za kiitikadi kwa vile uongozi wa takribani vyama vyote nya upinzani umetokana na kundi lilele la wanasiwa wa chama kikongwe na kinachoendelea kutawala - cha CCM. Maneno yaliyoibuka katika medani hii ni pamoja na:

- (1) uchumi wa soko huria.
- (2) ubinafsishaji
- (3) ubia
- (4) uzawa
- (5) zama za uwazi na ukweli.

#### **4.2 Msamiati unaohusu kuunga mkono vyama.**

Katika eneo hili msamiati mpya uliojitokeza unahusu mashabiki wa vyama nya kisiasa, k.m.

- (6) wakereketwa
- (7) wanamaskani
- (8) wafurukutwa
- (9) wakerwa.

#### **4.3 Msamiati unaohusu shughuli za kampeni.**

Kwa vile kampeni ni shughuli muhimu sana kwa vyama nya ushindani, eneo hili limezalisha msamiati mwangi wa Kiswahili. Hapa tutataja baadhi tu ya maneno mapya ama ya zamani lakini yaliyopatiwa maana mpya husianifu na shughuli za kampeni:

- (10) Mgombea mwenza
- (11) Mgombea (ubunge) kuititia/kwa tiketi ya (chama fulani)
- (12) Mpiga debe
- (13) Mpinzani mkuu (katika uchaguzi).

#### **4.4 Msamiati unaohusu nyadhifa.**

Vyama nya kisiasa vina nafasi za uongozi ndani ya vyama vyenyewe na pia katika vyombo nya uwakilishi, yaani Bungeni na katika Baraza la Wawakilishi,Zanzibar.Uongozi ndani ya vyama vyenyewe haukuzalisha msamiati wowote mpya kwani mfumo wa uongozi unaofuatwa na chama kinachotawala - CCM - ndiyo ulionakiliwa na vyama vipyta.Hata hivyo, katika vyombo nya uwakilishi nyadhifa mpya chache zimejitokeza na kuwakilishwa na msamiati mpya. Mifano:

- (14) Kiongozi wa Upinzani (Bungeni/ katika Baraza la Wawakilishi)
- (15) Mratibu wa Chama (Bungeni/Barazani)
- (16) Waziri Kivuli
- (17) Msemaji Mkuu wa Upande wa Upinzani.

### **5.0 Maoni ya Jumla kuhusu Msamiati Mpya wa Kisiasa**

Kuna mambo kadha ambayo yanaweza kusemwa kuhusiana na msamiati mpya uliojitokeza hivi karibuni kuelezea dhana mbalimbali za siasa ya vyama vingi.Kwanza kabisa ni kwamba karibu maneno yote mapya yametokana na Kiswahili chenyewe, yakiwa yamejengwa ama kuumbwa kwa "vijenzi" vilivyomo ndani ya lugha ya Kiswahili. Maneno ya mkopo toka lugha zilizoendelea k.v. Kiingereza hayakutumika.Hii ina maana kwamba karibu msamiati wote umetokana na

maneno " ya kawaida" (taz. pia Besha 1995) ambayo mjuzi yeote wa Kiswahili anaweza kuyatambua na kubaini maana zake za nyongeza (za kisiasa) kwa kutumia msingi wa maana za awali za maneno hayo anazozijua.Na kama alivyosema Besha (1995:68) ujenzi wa msamiati mpya kwa njia hii ndio msingi wenyewe wa ukaji wa lugha.Mwanajamii - lugha hupaswa daima kuongezea miundo ya awali anayojua kwa vile mashina ya maneno katika lugha kwa kawaida huwa machache sana ikilinganishwa na idadi kubwa na inayozidi kuongezeka ya dhana mpya (taz.Felber 1984:2).

Aidha matumizi ya Kiswahili chenyewe katika kuunda msamiati mpya wa kisiasa yanaonyesha ukomavu wa Kiswahili katika medani ya siasa. Ni uthibitisho kwamba Kiswahili kikipatiwa dhima ya kuhudumia eneo fulani la mawasiliano, kinao uwezo wa kuzalisha msamiati na istilahi mwafaka bila kutegemea kukopa sana kutoka kwenye lugha zilizoendelea.

Jambo la pili ni kwamba idadi kubwa zaidi ya msamiati mpya ulioundwa ni majina (nomino).Vitenzi ni vichache sana,k.m.

- (18) engua (Malecela ajiengua kugombea Urais)
- (19) kampenia (Nyerere kumkampenia Mkapa)
- (20) lipua (bomu) (Mrema alipua bomu jingine)
- (21) pigia (debe) (Rais aliyasema hayo alipokuwa anampigia debe mgombea wa kiti cha ubunge wa jimbo la Temeke kupitia chama cha CCM).

Jambo la tatu linahusu mbinu zilizotumika kuunda msamiati mpya wa kisiasa.Uchanganuzi wa data unaonyesha kuwa mbinu nne za uundaji maneno - unyambulishaji, 'uunganishaji wa maneno, upanuaji wa maana, na tafsiri sisisi<sup>3</sup> - ndizo zilizotumika zaidi katika kuzalisha maneno hayo mapya.Tutatoa mifano michache hapa chini:

- (i) Msamiati uliotokana na unyambulishaji:
  - (22) uzawa, mzawa < zaa
  - (23) upinzani, mpinzani < pinga
  - (24) mageuzi < geuka.
- (ii) Msamiati uliotokana na uunganishaji wa maneno:
  - (25) mgombea mwenza < mgombea + mwenza
  - (26) mlalahoi < mlala (=mtu lalaye) + hoi
  - (27) mpiga debe < mpiga (=mpigaji) + debe
- (iii) Msamiati uliotokana na upanuzi wa maana:
  - (28) mkereketwa < kereketa kt. 1. washa kooni au kinywani 2. udhi. (Yaani mshabiki wa CCM anayeudhiwa na changamoto toka vyama vipyta vya upinzaji)<sup>4</sup>.
  - (29) mfurukutwa < furukuta kt. 1. gaagaa kama vile kitandani mtu akiwa mgonjwa au akosapo usingizi 2. jaribu kujitoa uliposhikwa kwa nguvu. (Yaani mshabiki wa NCCR - Mageuzi anayejitutumua dhidi ya mashabiki wa chama tawala cha CCM).
  - (30) kigogo (vigogo). < gogo ji. kipande kikubwa cha mti ulioanguka au kukatwa. (Yaani mtu mwenye madara makubwa mahali pake pa kazi; kiongozi wa ngazi ya juu).
- (iv) Msamiati unaotokana na tafsiri sisisi:
  - (31) Msajili wa Vyama vya Siasa < Registrar of Political Parties.
  - (32) Kiongozi wa Upinzani < Leader of the Opposition.
  - (33) Kinyang'anyiro cha Urais < Scramble for the Presidency.

Jambo la mwisho linahusu uthabiti au uimara wa msamiati mpya uliobuniwa.Upembuzi wa makini wa msamiati uliojitekeza hivi karibuni katika medani ya siasa ya vyama vingi

unaonyesha kuwepo kwa makundi mawili ya msamiati huo. Kundi la kwanza ni lile linalotokana na maneno yanayotumika katika mazingira rasmi ya mawasiliano, yaani yanayotokana na Kiswahili sanifu.Haya ndiyo yale ambayo tayari yameshaingizwa kwenye hati rasmi za vyama, kama vile katiba, na pia kwenye vyombo vya uwakilishi,hususani Bungeni na katika Baraza la Wawakilishi.Mifano yake ni kama ile ya namba (10),(14), (15), (16),(17).Maneno haya tunaweza kusema kuwa tayari yamekwisha "sanifiwa" na yatakuwa na mashiko imara katika lugha ya Kiswahili. Hata kiwango cha matumizi yake ni cha juu, na kwa kawaida hutumiwa kwa ulinganifu na wanasiasa karibu wote, pasi na kuwepo visawe vya ziada. Hali hii ndiyo hasa inayopelekeea kwenye usanifishwaji wa msamiati wa kundi hili.

Kundi la pili la msamiati ni lile linalojumuisha maneno yanayotokana na misemo ya mitaani, yaani misimu ama simo.Mifano ya maneno haya ni pamoja na ile ya namba: (12), (20), (21),(26),(33). Kwa vile misimu aghalabu huwa na sifa ya kutoweka kutoka matumizini baada ya muda mfupi (taz.Mwansoko 1990) kuna uwezekano wa msamiati wa kundi hili kuteteraka na pengine hatimaye kutoweka.Hivyo kabla ya msamiati wa aina hii haujasanifishwa,itafaa udhihirishe uthabiti wake katika matumizi kwa walau miaka mitano.Mdee (1995) amependekenza kipindi cha "majaribio" ya msamiati wa namna hii kiwe miaka mitano hadi kumi.

## 6.0 Hitimisho

Tumedhihirisha katika makala hii kuwa lugha yoyote,Kiswahili kikiwemo,inapopatiwa dhima ya kuhudumia eneo jipya la mawasiliano inao uwezo wa kuzalisha msamiati na istilahi mwafaka za kuwakilishia dhana mpya husianifu na eneo hilo jipya la mawasiliano.Makala imeonyesha jinsi lugha ya Kiswahili ilivyomudu kujinyumbua na kuzalisha msamiati unaohitajika kufuatia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuingia kwenye mfumo wa siasa ya vyama vingi tangu mwaka 1992.Hata hivyo imetolewa hadhari kuwa sio maneno yote yaliyoundwa yana mashiko sawa kimatumizi katika medani ya siasa mamboleo ya ushindani.Maneno ya kisiasa yanayotokana na semi za mitaani (misimu) huenda yakatoweka baada ya muda mfupi kwa vile mwelekeo huo ni mojawapo ya nduni za misimu.

## Tanibihi.

- 1 Baadhi ya vyama hivi vilishiriki pia katika chaguzi ndogo zilizofanyika kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 1995.
- 2 Tafsili ya maneno yote yanayotumiwa kama mifano katika makala hii itatolewa kwenye Kiambatisho 1.
- 3 Kwa maelezo ya kina juu ya mbinu hizi za uundaji maneno tazama katika Tumbo-Masabo na Mwansoko (1992, Sura ya 4).
- 4 Maana za msingi za msamiati Na. 28, 29 na 30 zimetokana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI (1981).

## Marejeo

- Baraza la Wawakilishi, Zanzibar (1995) *Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar*, Toleo la mwaka 1995, Zanzibar, Idara ya Upigaji Chapa.
- Besha,R.M. (1995) "Nafasi ya Msamiati wa Magazeti katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu", katika J.G. Kjango na J.S. Mdee (Wah) *Utafiti na Utungaji wa Kamusi*,Dar es Salaam,TUKI:61 - 72.
- Felber,H. (1984) *Terminology Manual*, Paris,Infoterm /UNISIST/ UNESCO.

Ferguson, C.(1968) " Language Development", katika J.A.Fishman na wenzake (Wah) *Language Problems of Developing Nations*, New York, John Wiley & Sons, Inc.:27 - 36.

Mdee,J.S.(1995) " Misingi ya Uteuzi wa Vidahizo katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu",katika J.S. Mdee (Mh) *Misingi ya Utungaji Kamusi*,Dar es Salaam,TUKI:35 - 58.

Mwansoko,H.J.M. (1990) " Simo na Nafasi yake katika Kiswahili", katika *Mulika Na*.22:69 - 87.

Mwansoko, H.J.M. na Tumbo - Masabo, Z.N.Z. (1996) *Matumizi ya Kiswahili Bungeni*, Dar es Salaam, TUKI.

Nsekela,A.J. (1965) *Minara ya Historia ya Tanganyika hadi Tanzania*, Dar es Salaam, Longman Tanzania.

TUKI (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Nairobi, OUP.  
TUKI (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Nairobi, OUP.  
TUKI (1992) *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili*, Dar es Salaam,TUKI.

**Kiambatisho:** *Orodha ya baadhi ya msamiati mpya wa Kiswahili unaohusiana na mfumo wa siasa ya vyama vingi nchini Tanzania:*

Baraza la Mawaziri Vivuli - Baraza la Mawaziri wa Upande wa Upinzani.  
Binafisha (ubinafishaji) - fanya kiingizia mali cha umma k.v. kiwanda kiwe cha mtu au watu binafsi.

Chama cha upinzani - chama cha siasa ambacho hakipo madarakani.  
Chama tawala - chama ambacho kiko madarakani.

Duru la kwanza/la pili la uchaguzi - mzunguko wa kwanza wa uchaguzi/marudio ya uchaguzi huo endapo mshindi hakupatikana kwenye mzunguko wa kwanza.

Engua (enguliwa/jiengua) - toa katika kushindania kiti fulani; (tolewa katika kuwania nafasi fulani; jitoa kuwania kiti fulani).

Jibu mapigo - jitetea dhidi ya kashifa (uliozuliwa); toa majibu ya tuhuma dhidi yako.

Kampenia - pigia/ fanyia (mgombea) kampeni.  
Kinyang'anyiro (k.m. cha urais) - hali ya watu wengi kutaka kuwania/ kushindania nafasi fulani ya uongozi, mathalani Urais.

Kiongozi wa Upinzani (Bungeni au katika Baraza la Wawakilishi) - Mkuu wa Chama/Vyama vya Upinzani kuhusu mambo yote yanayohusu Bunge/ Baraza la Wawakilishi.

Lipua bomu - toa taarifa za kashfa dhidi ya kiongozi/viongozi wa chama ama serikali.  
Mageuzi - mabadiliko yanayotokana na marekebisho ya mfumo wa siasa nchini.

Maskani/Wanamaskani - mashabiki wa CCM wa Tanzania Visiwani.

Mdhalo wa wagombea kiti cha Urais - majadiliano maalumu ya ana kwa ana baina ya wagombea wa Urais wa vyama mbalimbali ambapo wagombea hao hueleza sera za vyama vyao na kujibu maswali toka kwa waandishi wa habari na wananchi wengine mashuhuri.

Mgombea (Urais/ Ubunge) kupitia/kwa tiketi ya (chama cha...) - anayewania kiti fulani kutokana na kuteuliwa kufanya hivyo na chama chake.Wakati wa mfumo wa chama kimoja usemi "... kupitia/kwa tiketi ya ..." haukuhitajika.

Mgombea mwenza - mgombea wa nafasi ya Umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mizengwe - vitendo vyta chinichini wakati wa zoezi la uchaguzi (kuanzia uteuzi wa wagombea hadi kuhesabu kura).

Mratibu wa Chama/Vyama vyta Upinzani (Bungeni/ katika Baraza la Wawakilishi) - Mdhibiti wa Wabunge/ Wawakilishi wa Upande wa Upinzani.

Msajili wa Vyama vyta Siasa - kiongozi mwenye dhamana ya kuviandikisha rasmi vyta vyta siasa.

Msemaji Mkoo wa Upande wa Upinzani - mchangiaji mkoo wa hoja fulani Bungeni/katika Baraza la Wawakilishi anayefanya hivyo kwa niaba ya wapinzani wote.

Pigia debe (wapiga debe) - fanyia mgombea kampeni; (wale wanaompigia mgombea fulani kampeni).

Sehemu yenyeye nguvu ya chama fulani - jimbo ambamo chama fulani kina nafasi kubwa ya kupata ushindi katika uchaguzi.

Ubia - umilikaji wa pamoja wa viingizia mali k.v. viwanda, makampuni; umilikaji huo huweza kuwa baina ya serikali na watu binafsi ama mionganoni mwa watu binafsi wenye.

Uchaguzi wa vyama vingi - uchaguzi (katika vyombo vyta uwakilishi) unaoshirikisha vyama kadhaa vyta kisiasa.

**Upinzani** (wapinzani; mpinzani mkoo) - mjumuiko wa wanasiada ambaa vyama vyao havimo madarakani, yaani haviongozi serikali. (Mpinzani mkoo ni mgombea wa chama kilichotishio zaidi kwa chama chako).

**Uzawa** (wazawa) - Utanzania wa asili kabisa; (Watanzania wa asili ya nchi hii kwa dhati yake, kinyume na wale ambaa asili yao si Tanzania ama Bara la Afrika kwa ujumla).

Vigogo - viongozi wa ngazi za juu kabisa wa (aghalaabu) vyama na serikali.

**Vyama vingi** - hali ambapo katika medani ya siasa huwepo chama zaidi ya kimoja. Hali iliyokinyume na ukiritimba wa chama kimoja.

Wafurukutwa - mashabiki wa chama cha NCCR - Mageuzi.

Wakereketwa - mashabiki wa CCM wa Tanzania Bara.

Wakerwa - mashabiki wa chama cha NLD.

Walalahoi - makabwela, watu wa tabaka la chini katika jamii.

**Wapambe** - wasaidizi wa kiongozi wa ngazi ya juu katika chama au serikali. Aghalaabu huandamana naye katika shughuli zake mbalimbali k.v. mikutano ya kampeni, ya kufungua matawi ya chama,n.k.

**Watazamaji/waangalizi** wa uchaguzi - mashirika yasiyo ya kiserikali au vikundi vyta watu vinavyofuatilia mwenendo wa hatua mbalimbali za uchaguzi ili kuona kama uko huru na ni wa haki. Mashirika na vikundi hivyo huweza kuwa vyta kitaifa ama kimaataifa.

**Waziri Kivuli** - miratibu na msemaji mkoo wa upande wa upinzani wa wizara (fulani mahususi).

**Zama za uwazi na ukweli** - enzi zisizo za kufichana uyakini wa mambo; enzi ambapo serikali itawaeleza wananchi bayana mambo yote wanayopaswa na wanayostahili kufahamishwa.